**HOTUBA YA IJUMAA**

**Israa na Miiraji na Ishara kubwa za Mwenyezi Mungu**.

Imefasiriwa

Na

Profesa Ayman Alasar

Shukrani zote za anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu Mwenye kusema ndani ya Kitabu chake Kitukufu:

**سُبْحَانَ الَّذِي أَسْرَى بِعَبْدِهِ لَيْلًا مِنَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ إِلَى الْمَسْجِدِ الْأَقْصَى الَّذِي بَارَكْنَا حَوْلَهُ لِنُرِيَهُ مِنْ آيَاتِنَا إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ.**

{**SUBHANA, Ametakasika aliye mchukua mja wake usiku mmoja kutoka Msikiti Mtukufu mpaka Msikiti wa Mbali, ambao tumevibariki vilivyo uzunguka, ili tumuoneshe baadhi ya Ishara zetu. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia na Mwenye kuona**}. Ninashuhudia kuwa hakuna mola wa haki isipokuwa ni Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika, na ninashuhudia kuwa Mtume wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake. Ewe Mwenyezi Mungu peleka rehma amani na baraka kwake pamoja na kwa watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake na wale wote waliowafuata kwa wema mpaka siku ya malipo.

**Baada ya Utangulizi**:

Ndugu zangu wislamu Kwa hakika Safari ya Israa na Miiraji ni muujiza mkubwa unaonesha kiwango cha uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwani Yeye Mwenyezi Mungu ndio Muumba wa sababu na vinavyosababisha, wala haikuwa ajabu kwa watu wala ajabu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwani Mwenyezi Mungu kama katika kauli yake (s.w):

**إِنَّمَا أَمْرُهُ إِذَا أَرَادَ شَيْئًا أَنْ يَقُولَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ.**

{**Hakika amri yake anapo taka kitu ni kukiambia tu: Kuwa! Na kikawa**}.

Mwenyezi Mungu katika safari hii tukufu alimpendelea kipenzi cheka Mtume Muhammad S.A.W ambapo alimpandisha kutoka kwenye ulimwengu huu wa ardhi na kumpeleka kwenye ulimwengu wa mbinguni, na kumfikisha mpaka eneo la Sidratul-Muntaha ili kumuonesha alama kubwa za uwepo wake na maajabu ya uwezo wake mkubwa Mola Mtukufu.

Katika alama zake hizi kubwa miongoni mwao zipo tulizojifunza na zengine hatujajifunza ambapo Mwenyezi Mungu alimpeleka Mtume wake S.A.W wakati wa usiku kutoka Msikiti Mtakatifu wa Makka kwenda Msikiti Mtakatifu wa Al-Aqswa, kisha baada ya hapo alimpandisha kwenda mbinguni na baadaye kumrudisha kutoka mbinguni kumpeleka tena Msikiti Mtakatifu wa Al-Aqswa na mwisho kabisa kumrudisha kwa mara nyengine Msikiti Mtakatifu wa Makka yote hayo ndani ya usiku mmoja, kwa kweli ni uwezo tu wa Mwenyezi Mungu na si vyengine.

Mtume wetu S.A.W aliona katika ufalme wa mbinguni maajabu ya uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu ambao hajawahi kuona, na Quran inatuelezea alama kubwa za Mwenyezi Mungu ambapo Mola Mtukufu Anasema:

سَنُرِيهِمْ آيَاتِنَا في الآفَاقِ وفِي أَنْفُسِهِمْ حَتَّى يَتَبَيَّنَ لَهُمْ أَنَّهُ الحَقُّ .

{**Tutawaonesha Ishara zetu katika upeo wa mbali na katika nafsi zao wenyewe mpaka iwabainikie kwamba haya ni kweli**}.

Na miongoni mwa Ishara hizi kubwa ni pamoja na Mwenyezi Mungu kumuwezesha mnyama aina ya Buraku kwa Mtume wetu SAW ambapo Mtume anasema:

أُتيتُ بالبُراقِ، وهو دابَّةٌ أبيضُ طويلٌ، يضعُ حافرَه عند مُنتهَى طرْفِه.

"*Nilimpanda Buraku, naye ni mnyama mrefu mweupe, anaweka kwato yake pale linapoishia kuona jicho lake*" katika hili kuna dalili ya uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kama vile kuna mafundisho kwa Mtume SAW ya kuchukuwa sababu katika mambo, kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu alikuwa na uwezo wa kumpeleka Mtume wake ndani ya usiku ule bila ya kutumia njia yeyote wala sababu.

Pia Miongoni mwa Ishara: Ni kukutana kwake Mtume S.A.W na Manabii na Mitume ambapo uwezo wa Mwenyezi Mungu ulijipambanua kwenye kuwarudishia uhai ambapo waliswali nyuma ya Mtume SAW ndani ya Msikiti wa Al-Aqswa, na alifanikiwa kukutana na aliyokutana nao huko mbinguni, wote walimkaribisha na kumuombea duwa za kheir, na hii ni utekelezaji wao wa ahadi zao na makubaliano yao na Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kauli yake Mola Mtukufu:

**وإِذْ أَخَذَ اللَّهُ مِيثَاقَ النَّبِيِّينَ لَمَا آتَيْتُكُمْ مِنْ كِتَابٍ وَحِكْمَةٍ ثُمَّ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مُصَدِّقٌ لِمَا مَعَكُمْ لَتُؤْمِنُنَّ بِهِ وَلَتَنْصُرُنَّهُ قَالَ أَأَقْرَرْتُمْ وَأَخَذْتُمْ عَلَى ذَلِكُمْ إِصْرِي قَالُوا أَقْرَرْنَا قَالَ فَاشْهَدُوا وَأَنَا مَعَكُمْ مِنَ الشَّاهِدِينَ .**

{**Na pale Mwenyezi Mungu alipo chukua ahadi kwa Manabii: Nikisha kupeni Kitabu na hekima, kisha akakujieni Mtume mwenye kusadikisha mliyo nayo, ni juu yenu mumuamini na mumsaidie. Akasema: Je, mmekiri na mmekubali kushika agizo langu juu ya hayo? Wakasema: Tumekubali. Akasema: Basi shuhudieni, na Mimi ni pamoja nanyi katika kushuhudia**}.

Miongoni pia mwa Ishara au alama: Ni Mtume SAW kuiona Baiti Al-Maamur huko mbinguni, ambapo anasema Mtume SAW:

**فإذا أنا بإبراهيمَ مُسنِدًا ظهرَه إلى البيتِ المعمورِ، وَإِذَا هُوَ يَدْخُلُهُ كُلَّ يَوْمٍ سَبْعُونَ أَلْفَ ملَكٍ، لا يَعُودُونَ إِلَيْهِ.**

"*Mara nikamuona Nabii Ibrahimu ukiwa mgongo wake ameuegemesha Baitul-Maamur, ndani yake wanaingia Malaika elfu sabini kila siku na wala hawarudi*".

Na Mwenyezi Mungu Ameapa ndani ya Quran kwa heshima yake na ukubwa wake ambapo Anasema Mola Mtukufu: **وَالبَيْتِ المَعْمُورِ** {**Na kwa Nyumba iliyo jengwa**}.

Na katika Ishara pia: Ni Mtume SAW kufika eneo la Sidratul-Muntaha, na hii ni takrimu ya Mwenyezi Mungu kwa Mtume wetu SAW ambapo Mola Mtukufu Anasema:

مَا كَذَبَ الْفُؤَادُ مَا رَأَى * أَفَتُمَارُونَهُ عَلَى مَا يَرَى * وَلَقَدْ رَآهُ نَزْلَةً أُخْرَى * عِنْدَ سِدْرَةِ الْمُنْتَهَى * عِنْدَهَا جَنَّةُ الْمَأْوَى * إِذْ يَغْشَى السِّدْرَةَ مَا يَغْشَى.

{**Moyo haukusema uwongo uliyo yaona * Mnabishana naye kwa aliyo yaona? * Na akamuona mara nyengine * Penye Mkunazi wa mwisho * Karibu yake ndiyo ipo Bustani inayo kaliwa * Kilipo ufunika huo Mkunazi hicho kilicho ufunika**}.

****

**HOTUBA YA PILI:**

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, rehma na amani zimwendee Mtume wa mwisho naye ni Mtume Muhammad SAW pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake wote.

Safari ya Israa na Miiraji ilikuwa ni sehemu ya kukirimiwa kwa Mtume wetu Muhammad SAW baada ya kufikwa na mitihani mingumu, ili kuwa ni zawadi ya kuondoa huzuni na kuuthibitisha moyo wake pamoja na kuituliza nafsi, ambapo Mola Mtukufu Anasema: **فَإِنَّ مَعَ العُسْرِ يُسْرًا * إِنَّ مَعَ العُسْرِ يُسْرًا** {**Basi kwa hakika pamoja na uzito upo wepesi * Hakika pamoja na uzito upo wepesi**}.

Mwenyezi Mungu Mtukufu alimuonesha Mtume wake mambo mengi ya ajabu na siri za kiulimwengu ikiwa ni kumjulisha yeye Mtume kuwa yupo pamoja na Mwenyezi Mungu Mtukufu na yupo katika ulezi wake na kinga yake, kama alivyosema Imamu Al-Buswiry:

Umepelekwa usiku kutoka sehemu takatifu kwenda sehemu takatifu - - Kama vile unavyopelekwa mbaramwezi katika kiza kinene.

Ukaendelea kupandishwa mpaka ukafikia sehemu - - kati ya pinde mbili au karibu zaidi hukufahamu wala wahi kuiona.

Ukaletewa Manabii wote - - Na Mitume ikiwa kutangulizwa muhudumiwa kwenye huduma.

Ewe Mwenyezi Mungu turuzuku liwazo njema kwa Nabii wako S.A.W duniani na utupatia uombezi wake siku ya mwisho.

AMIN